

**HOTUBA YA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA
MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB) AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA
KWA MWAKA 2018/2019**

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

2. **Mheshimiwa Spika**, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2018/19 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, namshukuru kwa dhati **Mhe.Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini kuendelea kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Vilevile, napenda kuwashukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mhe.Dkt. Ali Mohamed Shein** na Waziri Mkuu, **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** kwa uongozi wao makini na maelekezo wanayoyatoa katika kufanikisha utendaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na

Usalama ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Azzan Mussa Zungu (Mb)** na wajumbe walioteuliwa katika Kamati hii. Naishukuru sana Kamati kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kuiongoza vyema Wizara. Kwa kipindi chote imetoa ushauri, imesimamia, imefuatilia kwa kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara. Kwa kufanya hivyo, Kamati imeweza kuona maendeleo na changamoto za utekelezaji wa miradi hiyo na kutoa ushauri na maelekezo stahiki ya namna ya kukabiliana nazo. Ushauri na maelekezo yao wakati wakichambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2018/19 yamesaidia sana katika kuandaa Mpango na Bajeti hii.

4. **Mheshimiwa Spika**, aidha, nitumie fursa hii pia kumpongeza Luteni Jenerali Yacoub Hassan Mohamed kwa kupandishwa cheo na kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Pia, napenda kuwapongeza Luteni Jenerali Paul Peter Masao, Mkuu wa Chuo cha kijeshi - Monduli kwa kupandishwa cheo, Meja Jenerali Martin Shiminzi Busungu, kwa kupandishwa cheo na kuteuliwa kuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, na Meja Jenerali Sharif Sheikh Othman kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Kamandi ya Vikosi chini ya Makao Makuu ya Jeshi. Kipekee, napenda kuwashukuru Luteni Jenerali Mstaafu James Aloyce Mwakibolwa, aliyekuwa Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Meja Jenerali Mstaafu Michael Joseph Isamuhyo, aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kulitumikia Jeshi kwa ufanisi na mafanikio makubwa.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwapongeza makamanda wafuatao waliopandishwa vyeo kuwa Meja Jenerali na kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa

Tanzania: Meja Jenerali Blasius Kalima Masanja, Mkuu wa Utumishi Jeshini; Meja Jenerali George Thomas Msongole, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavuu; Meja Jenerali Alfred Fabian Kapinga, Mkuu wa Operesheni na Mafunzo; Meja Jenerali Mathew Edward Mkingule, Mdhibiti Mkuu wa Jeshi; Meja Jenerali Kaisy Philip Njelekela, Jaji Wakili Mkuu; Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu, Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi; Meja Jenerali Anselm Shigongo Bahati, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la “Tanzania Automotive Technology Centre” (TATC - Nyumbu), Meja Jenerali Shija Seif Makona, Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga na Meja Jenerali Ramadhan Rama Mrangira, Kamishna wa Utafiti na Maendeleo ya Jeshi. Wote kwa ujumla wao nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao.

6. **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika chaguzi ndogo kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni; Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini; Mhe. Maulid Mtulia, Mbunge wa Kinondoni; Mhe. Dkt. Godwin Mollé, Mbunge wa Siha; Mhe. Justine Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini; na Mhe. Dkt. Stephen Kiruswa, Mbunge wa Longido. Wote kwa ujumla, pamoja na pongezi hizi, nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu muhimu ya Mhimili wa Bunge na ya kuwatumikia wananchi wa majimbo yenu.

7. **Mheshimiwa Spika**, ninaungana na wenzangu kutoa salamu za pole kwako Mhe. Spika, Bunge lako Tukufu, familia na wananchi wote wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuondokewa na mwenzetu Mhe. Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini kupitia Chama cha Mapinduzi. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho ya marehemu mahali pema. Amina.

8. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, natoa pole kwa wale waliopatwa na majanga, pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini yakiwemo mafuriko na ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema na kuwajalia majeruhi wote kupona haraka na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

9. **Mheshimiwa Spika**, kipekee natoa pole kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Maafisa, Askari na familia za Wanajeshi 19 waliopoteza maisha wakitekeleza jukumu la ulinzi wa amani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) mnamo mwezi Septemba, Oktoba na Desemba, 2017. Nawaombea marehemu walale mahali pema. Napenda kuwaombea majeruhi wote wa mashambulizi hayo afya zao ziendeele kuimarika.

DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

10. **Mheshimiwa Spika**, **Dira** ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu. Vivyo hivyo, **Dhima** ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi ya nchi yetu yanakuwa salama.

11. **Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha **Dira** na **Dhima**, Wizara imeendelea kuwa na malengo yafuatayo:

- (i) Kuwa na Jeshi dogo lenye wataalam, zana na vifaa vya kisasa;

- (ii) Kuwajengea vijana wa kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa na kuwafundisha stadi za kazi;
- (iii) Kuendeleza tafiti na kujenga uwezo katika teknolojia kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;
- (iv) Kuwa na Jeshi imara la akiba;
- (v) Kuwa chombo cha msaada kwa mamlaka za kiraia katika kukabiliana na athari za majanga na matukio yanayoweza kuhatarisha amani na utulivu nchini; na
- (vi) Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

12. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili iweze kufikia malengo yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Kulipatia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania wataalam, vifaa na zana bora pamoja na kutoa mafunzo kwa Wanajeshi ili kuliongezea uwezo wa kiutendaji kivita;
- (ii) Kuboresha mazingira ya kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahili na mahitaji ya msingi kwa Wanajeshi na Watumishi Raia;
- (iii) Kuwapatia vijana wa kitanzania mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi;
- (iv) Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia; na
- (v) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

13. **Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2017/18 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kwa Wizara yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huo pia zimezingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/19 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2015-2020

14. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ya mwaka 2015-2020 kwa pamoja na utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara. Majukumu hayo yameainishwa kwenye ibara ya 146 katika vifungu vifuatavyo:

- (i) Kuviwezesha vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha;
- (ii) Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama;
- (iii) Kuendelea kuweka mazingira mazuri yanayoliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha mafunzo kwa vijana

wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa mujibu wa sheria;

- (iv) Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika shughuli za Ulinzi wa Amani kwenye nchi mbalimbali duniani ili majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani; na
- (vi) Kuendelea kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka (Cross Border Crimes) hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji wa fedha haramu (Money Laundering), biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji wa binadamu.

Maelezo ya utekelezaji wa majukumu hayo yamebainishwa katika **Kiambatisho Na.1.**

HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

15. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya usalama wa mipaka yetu kwa ujumla imeendelea kuwa shwari. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 hakuna matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), limeendelea kutekeleza majukumu yake ya ulinzi wa mipaka na mengine yanayotolewa kwa mujibu wa sheria kwa weledi na umakini, ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama. Hata hivyo, kuendelea kuwepo kwa migogoro na viashiria vya machafuko ya ndani katika baadhi ya nchi tunazopakana nazo, kumesababisha ongezeko la wakimbizi na wahalifu wanaoingia nchini, wakiwemo wenye silaha za moto na kuzitumia silaha hizo katika uhalifu.

16. **Mheshimiwa Spika**, tatizo la uharibifu wa alama za mipaka bado lipo. Juhudi za Serikali yetu kwa pamoja na nchi husika zimeendelea kutafutiwa ufumbuzi wa changamoto hiyo, hususan katika mpaka wa Kaskazini tunakopakana na nchi za Kenya na Uganda. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeendelea na mazungumzo na nchi tunazopakana nazo ili kutatua changamoto za mipaka, ikiwemo uwekaji wa alama za mipaka (boundary pillars) zilizoharibiwa na uwekaji wa alama mpya za mipaka katika maeneo yanayohitaji kuwekwa alama hizo ili kuimarisha ulinzi. Maelezo ya kina ya hali ya mipaka yetu ni kama ifuatavyo:

Mpaka wa Mashariki

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mpaka huu Tanzania inapakana na Bahari ya Hindi na hali ya usalama katika mpaka huu ni shwari. Changamoto zilizopo katika mpaka huu ni uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi, kuwepo kwa biashara za magendo na kutumika kama mapitio ya wahamiaji haramu, wasafirishaji wa madawa ya kulevyo na usafirishaji haramu wa binadamu. JWTZ linakabiliana na changamoto hizo kwa kutumia vikosi vya Jeshi la Wanamaji vikisaidiana na vikosi vya Jeshi la Nchi Kavu na Anga na wadau wengine kufanya doria na kuendesha operesheni za ulinzi katika eneo letu la bahari. Pia, JWTZ limekuwa likifanya doria za pamoja za mara kwa mara na majeshi ya nchi ya Msumbiji na Afrika Kusini.

Mpaka wa Kaskazini

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mpaka huu Tanzania imepakana na nchi za Kenya na Uganda na hali ya usalama katika mpaka huu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya uwazi wa mpaka (porous border), hali ambayo inaweza kuchochea uwezekano wa wahalifu kuingia nchini na kuhatarisha usalama wa nchi, kuharibika kwa baadhi ya alama za mipaka (boundary pillars) na baadhi ya maeneo kuwa na nafasi kubwa kati ya alama moja na nyingine. Serikali za Tanzania na Kenya zimefanya uhakiki ili kuimarisha mipaka ambapo awamu ya kwanza yenye urefu wa kilomita 238 imehusisha eneo kuanzia Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron. Kamati ya pamoja ya ufundi imefanya vikao na kutoa mafunzo kwa wajumbe kwa ajili ya kuelimisha wananchi waishio mipakani waelewe na kusaidia utunzaji wa alama za mipaka.

19. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania na Uganda zimeafikiana kufanya mapitio ya mpaka kwa lengo la kurejesha alama zilizong'olewa na kuweka alama mpya pale ambapo nafasi kati ya alama moja hadi nyingine ni kubwa. Changamoto ya eneo hili ni kukosekana kwa mkuza kutokana na ujenzi holela na shughuli za kijamii zinazofanywa katika maeneo ya mpaka huo. Wataalam wetu wanaendelea na majadiliano na wenzao wa Kenya na Uganda kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo. Baadhi ya wafugaji wa nchi jirani huingiza mifugo upande wa Tanzania kutafuta malisho na maji kinyume cha sheria. Vilevile, ipo changamoto katika mpaka ndani ya Ziwa Victoria kutokana na wananchi wa pande zote kuingiza na kusafirisha bidhaa nje ya nchi kwa njia ya magendo, hali hii inaikosha nchi mapato yanayotokana na kodi. Eneo hilo pia limekuwa likitumika kupitisha dawa za kulevya, silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria ambazo hutumika kufanya

uhalifu, na uvuvi haramu unaofanywa na raia wa Tanzania na nchi jirani. Aidha, wavuvi wa Tanzania hubughudhiwa na wahalifu kutoka nchi jirani kwa kuporwa samaki, fedha, vifaa na zana za uvuvi.

20. **Mheshimiwa Spika**, tatizo la wahamiaji haramu na usafirishaji wa binadamu kutoka nchi za Somalia, Eritrea na Ethiopia kuingia nchini limeendelea kuwepo. Mara nyingi uhalifu huu umekuwa ukifanyika kupitia mpaka wetu na Kenya kwa kutumia mawakala ambao wana mtandao mkubwa unaohusisha baadhi ya raia wa Tanzania na raia wa nchi wanazopitia. Aidha, ubovu wa miundombinu ya barabara za usalama mpakani unachangia maeneo hayo kutofikika kwa urahisi na hivyo kurahisisha uhalifu huo kufanyika. Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizi ni pamoja na kuimarisha ulinzi katika Ziwa Victoria pamoja na kufanya vikao vya ujirani mwema vya viongozi wa maeneo ya mpakani.

Mpaka wa Magharibi

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mpaka huu Tanzania imepakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama katika mpaka huu ni shwari. Changamoto katika mpaka huu ni pamoja na kuwepo kwa vikundi vya waasi vyenye silaha eneo la Mashariki mwa DRC na hivyo kutishia usalama kwa nchi za Maziwa Makuu ikiwemo Tanzania. Baadhi ya wahalifu kutoka nchi jirani wamekuwa wakivuka mpaka huo na kuingia upande wa Tanzania kufanya uporaji wa kutumia silaha na kuhatarisha usalama. Kwa upande mwingine machafuko yanayotokea DRC yamesababisha wimbi la wakimbizi kuingia hapa nchini. Aidha, uharibifu wa

baadhi ya alama za mpaka baina ya Tanzania na Burundi umeendelea kuwa changamoto ambayo imeanza kupatiwa ufumbuzi wa pamoja.

22. **Mheshimiwa Spika**, katika mpaka wa Tanzania na Rwanda kumekuwa na tatizo la uvuvi haramu katika Mto Kagera na Ziwa Ngoma unaofanywa na raia wa nchi jirani. Aidha, kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wavuvi wa Tanzania kufanyiwa vitendo viovu na wahalifu wanaosadikiwa kutoka nchi jirani. Matukio ya baadhi ya wafugaji kutoka nchi jirani kuingiza mifugo nchini kinyume cha sheria yameendelea kujitokeza. Pia, baadhi ya wafugaji hao wamekuwa wakiingiza mifugo yao kwenye hifadhi za Taifa na mapori ya akiba. Hatua zinazochukuliwa kukabili changamoto hizo ni pamoja na kufanya vikao vya ujirani mwema katika maeneo ya mpaka huo ili kuwapa fursa viongozi wa maeneo hayo kujadili na kupata ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hizo. JWTZ limeendelea kuimarisha doria pamoja na kuvijengea uwezo vikosi na viteule vilivyoko katika mpaka huu.

Mpaka wa Kusini

23. **Mheshimiwa Spika**, mpaka huu Tanzania inapakana na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia na hali ya ulinzi na usalama kwa ujumla ni shwari. Changamoto zilizopo ni pamoja na maeneo mengine ya mpaka kuwa wazi, uharibifu wa baadhi ya alama za mpaka, ujenzi holela, ubovu wa miundombinu ya barabara za kuzunguka mpaka, biashara za magendo na uhamiaji haramu. Katika upande wa mpaka wa Msumbiji hivi karibuni, kumejitokeza matukio yaliyofanywa na vikundi vya kihalifu. Aidha, kumekuwa na taarifa ya baadhi ya wahalifu kuvuka mpaka na kuingia Tanzania na kutoka Tanzania kuingia Msumbiji kufanya uhalifu au

kutafuta maficho. JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vya Tanzania na Jeshi la Msumbiji yamefanya vikao kujadili suala hili na kulitafutia suluhu.

24. **Mheshimiwa Spika**, mgogoro wa mpaka baina ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa bado haujapatiwa ufumbuzi. Juhudi za pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Malawi zinaendelea chini ya usuluhishi wa Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), ili kupata ufumbuzi wa mgogoro huo kwa njia ya amani. Kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Zambia kuna changamoto ya ujenzi holela katika eneo la Tunduma. Ujenzi huo umefanyika hadi ndani ya eneo la mkuza, ambalo linapaswa kuwa wazi kulingana na makubaliano kati ya nchi na nchi. Hatua zinazochukuliwa kukabili changamoto hizi ni pamoja na kuendelea kuimarisha vikosi na viteule vilivyo jirani na mpaka huu, na pia kuanzisha vikosi na viteule katika maeneo yenye uhitaji na kufanyika vikao vya pamoja na wataalam wa mamlaka zenye dhamana ya ardhi wa Tanzania na Zambia.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/18

25. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Wizara ilikadiriya kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 69,706,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu ya NGOME Fungu-38 **Shilingi 15,601,000.00**, JKT Fungu-39 **Shilingi 54,003,000.00** na Wizara Fungu-57 **Shilingi 102,000.00**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 mafungu hayo yaliweza kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 62,120,242.00** sawa na asilimia **89.12** ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38 –NGOME, ilikusanya jumla ya **Shilingi 21,305,042.00** zilizotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na kamisheni zinazotokana na JWTZ

kuwa wakala wa ukusanyaji wa makato ya bima zinazokatwa kwa Wanajeshi kutoka kampuni mbalimbali za Bima. Fungu 39 - JKT lilikusanya **Shilingi 40,215,200.00** kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mazao ya bustani (mboga mboga na matunda), mazao ya mifugo na mazao ya shambani. Fungu 57 - Wizara limekusanya kiasi cha **Shilingi 600,000.00** ambazo zimetokana na kodi ya pango la kantini.

26. **Mheshimiwa Spika**, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/18, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 1,725,517,816,925.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,506,517,816,925.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 219,000,000,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeoneshwa katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Bajeti ya Mwaka 2017/18

FUNGU	MATUMIZI		
	KAWAIDA	MAENDELEO	JUMLA
38-NGOME	1,205,244,289,563.00	8,000,000,000.00	1,197,543,710,510.00
39 - JKT	283,362,530,783.00	6,000,000,000.00	290,034,214,000.00
57 - Wizara	17,910,996,579.00	205,000,000,000.00	249,000,178,000.00
Jumla	1,505,517,816,925.00	219,000,000,000.00	1,725,517,816,925.00

27. **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2018 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,460,297,850,142.38** sawa na **asilimia 84.63** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo

Shilingi 1,278,717,774,796.50 sawa na **asilimia 84.94** ya bajeti iliyoidhinishwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 181,580,075,345.88** sawa na **asilimia 82.91** ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Mchanganuo wa bajeti hiyo kwa mafungu yote matatu na kiasi kilichopokelewa hadi mwezi Aprili, 2018 umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

28. **Mheshimiwa Spika**, fedha za matumizi ya kawaida zimetumika kulipa mishahara na posho kwa Watumishi wa Umma na Wanajeshi, kugharamia posho ya chakula cha maafisa, askari na vijana wa mujibu wa sheria, kulipa sehemu ya madeni ya wazabuni wanaotoa huduma na kulipa madeni ya maafisa, askari na watumishi raia. Aidha, fedha hizo zimetumika katika shughuli za kijeshi na kiulinzi katika nchi za Kikanda, mazoezi, mafunzo na operesheni za kijeshi, kulipia vikao vya kisheria vya ukaguzi na bodi ya manunuzi pamoja na uendeshaji wa ofisi.

29. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya maendeleo **Shilingi 181,580,075,345.88** zilizotolewa kupitia mafungu yake yote matatu zimetumika kulipia ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi, malighafi kwa ajili ya kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi katika Shirika la Mzinga, kuendeleza shughuli za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia katika Shirika la TATC (Nyumbu), ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule na vyuo vya kijeshi.

30. **Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote matatu ya Wizara, hususan fedha za mishahara na chakula katika kipindi hicho ulikuwa wa kuridhisha. Fedha kwa ajili ya mishahara na marupurupu zilipokelewa kulingana na makisio ya bajeti. Kwa upande wa fedha za maendeleo, kumekuwa na changamoto ya

fedha zilizopokelewa kutokidhi mahitaji na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na ulipaji wa madeni ya kimikataba. Wizara inaamini kwamba fedha zilizosalia zitapatikana kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2017/18.

MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/18

Matumizi katika Shughuli za Kawaida

31. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara imefanikiwa kulipa kwa wakati mishahara na posho zinazoambatana na mishahara na fedha za chakula kwa Wanajeshi. Aidha, fedha nyingine zimetumika kufanikisha sherehe mbalimbali za maadhimisho ya kijeshi na kitaifa, ushiriki wa timu za Jeshi katika michezo ya majeshi ya nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki pamoja na kutekeleza majukumu mengine yafuatayo:-

Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi

32. **Mheshimiwa Spika**, mafunzo mbalimbali yameendelea kutolewa katika shule na vyo vya kijeshi ndani na nje ya nchi, vikiwemo Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC-Duluti, Arusha), Chuo cha Uongozi wa Maafisa (TMA), Chuo cha *High Commanders Defence Studies* (HCDS), Shule ya Mafunzo ya Huduma na Utawala (SMH-Pangawe), na Shule za Mafunzo ya Awali na Uongozi kwa Askari. Aidha, maafisa na askari wameendelea kupata mafunzo katika nchi mbalimbali zikiwemo Afrika Kusini, Bangladesh, Burundi, Canada, China, Cuba, Ghana, India, Israel, Jamaica, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Morocco,

Nigeria, Oman, Pakistan, Rwanda, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Zambia na Zimbabwe.

33. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Jeshi lilifanikiwa kufanya mazoezi mbalimbali ya kitaifa na ya kimataifa yafuatayo; **Ex-Matumbawe** lilifanyika Mkoani Tanga tarehe 16 Julai hadi 30 Agosti, 2017 likihusisha nchi ya Tanzania, Zimbabwe, Zambia, Malawi, Afrika ya Kusini na Lesotho, **Ex-Blue Kunene** lilifanyika nchini Namibia kuanzia tarehe 24 Agosti hadi 02 Septemba, 2017 likishirikisha majeshi ya anga kwa wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na **Ex - Ushirikiano Imara** lililofanyika “*Peace Keeping Training Centre*” (PTC)-Kunduchi, Dar es Salaam kuanzia tarehe 04 hadi 20 Desemba, 2017 likihusisha nchi za Afrika Mashariki. Mafunzo na mazoezi yanayotolewa yanaliwezesha Jeshi kuongeza uwezo wake kiutendaji.

Mafunzo ya Jeshi la Akiba

34. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limetoa mafunzo kwa Jeshi la Akiba kwa wananchi katika ngazi ya awali. Jumla ya wananchi 19,016 wamepata mafunzo hayo, kati yao 16,595 ni wanaume na 2,421 ni wanawake. Hili ni ongezeko la wahitimu 5,019 sawa na asilimia 35.6 ya wananchi 13,997 waliopata mafunzo hayo mwaka 2016/17. Mafunzo haya yamefanyika katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Huduma za Afya na Tiba

35. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa maafisa, askari, watumishi wa umma, familia zao na wananchi kwa ujumla. Pamoja na upatikanaji wa huduma hizo kwa Wanajeshi, takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka 2017/18 hospitali za Jeshi zilitoa huduma za matibabu kwa wananchi 282,902. Hatua zinazochukuliwa na Wizara kuboresha huduma za afya ni pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba ili kukidhi mahitaji ya hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Hospitali za Kanda na vituo vya tiba vikosini. Aidha, mapendekezo ya kuboresha zaidi huduma za matibabu kwa Wanajeshi yameandaliwa na mara baada ya kukamilika yatawasilishwa serikalini kwa uamuzi. Utaratibu wa matibabu unaoandaliwa utaliwezesha Jeshi kutoa huduma bora na za uhakika kwa Wanajeshi walio katika utumishi na baadaye wastaafu baada ya mapendekezo hayo kuridhiwa.

Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine

36. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na za Kimataifa hususan katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa. Kikosi kimoja cha Jeshi kipo Darfur nchini Sudan chini ya mpango wa *United Nations - Africa Union Mission in Darfur* (UNAMID). Kikosi cha pili kipo Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) katika mpango wa *United Nations Organization Stabilization in Democratic Republic of Congo* (MONUSCO) kama sehemu ya MONUSCO Force Intervention Brigade - FIB. Kikosi cha tatu kipo katika nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati katika mpango wa *United Nations Multidimensional*

Integrated Stabilization Mission in the Central African Republic (MINUSCA) kikiwa sehemu ya MINUSCA na Kombania mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanon chini ya mpango wa kulinda amani chini ya mpango wa *United Nations Interim Force in Lebanon* (UNIFIL). Jeshi linategemea kupeleka Kombania ya wahandisi wa medani (Combat Engineers) nchini Sudani Kusini baada ya kukamilika kwa makubaliano ya kimkataba (Memorandum of Understanding) baina ya Serikali ya Tanzania na Umoja wa Mataifa. Aidha, Jeshi linao Maafisa Wanadhimu na Makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Sudan, Sudani Kusini, Ivory Coast, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na DRC. Vilevile, Jeshi limekuwa likishiriki katika vikao mbalimbali vya kikanda ikiwemo mikutano ya AU, EAC, SADC na nchi za eneo la Maziwa Makuu.

37. **Mheshimiwa Spika**, mnamo mwezi Septemba, Oktoba na Desemba, 2017 vikosi vyetu vikiwa katika jukumu la ulinzi wa amani nchini DRC maeneo ya Mamondioma na Simulike vilishambuliwa na makundi ya waasi kwa nyakati tofauti na kusababisha wanajeshi wetu 19 kupoteza maisha na wengine 66 kujeruhiwa. Maafa yaliyotokea kwa wanajeshi hayakusababishwa na ukosefu wa mafunzo. Maafisa na Askari hao walipata mafunzo ya kutosha kabla ya kwenda na waliendelea kupata mafunzo zaidi wakiwa katika eneo la Operesheni. Kushambuliwa kwao na kupoteza maisha ni kwa sababu waasi wa “Allied Democratic Forces” (ADF) walifanya shambulio la kushtukiza wakiwa na nguvu kubwa, na pia maafisa na askari wetu walichelewa kupata msaada stahiki kwa wakati kutoka MONUSCO. Timu ya Uchunguzi ya Umoja wa Mataifa imefanya uchunguzi na mapendekezo ya Timu hiyo yanafanyiwa kazi na wadau mbalimbali kwa kadiri

yanavyowahusu, ikiwemo Umoja wa Mataifa, MONUSCO na Serikali ya Tanzania.

38. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na matukio hayo ya kusikitisha, wanajeshi wetu hawakuvunjika moyo walizidi kuwa jasiri na kuendelea na majukumu yao. Hatua zilizochukuliwa na Jeshi ni pamoja na kupeleka maafisa na askari kuziba pengo lililoachwa na askari waliopoteza maisha na kujeruhiwa kulingana na taratibu za kijeshi, kuimarisha mafunzo kwa wanajeshi wanaoandaliwa kwenda kwenye Operesheni za Ulinzi wa Amani, na kukamilisha nyaraka za Umoja wa Mataifa na za ndani ya nchi kuhusu stahiki za marehemu na majeruhi wa shambulizi hilo.

Ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia

39. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za kusaidia Mamlaka za kiraia wakati wa maafa ikiwemo; kuchimba mfereji wa urefu wa kilomita 2 wa kuchepusha maji kunusuru wananchi wa eneo la Kilosa Mkoani Morogoro dhidi ya mafuriko yaliyotokea mwezi Januari, 2018. Aidha, Jeshi lilishiriki katika uokoaji wa wananchi waliokumbwa na mafuriko katika eneo hilo na kuwasaidia kupata makazi ya muda katika Kata za Tindiga na Malui.

40. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu yake ya msingi JWTZ limehusika katika kuhamisha Wizara na Idara mbalimbali za Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kwa kutumia magari yake, kusafirisha mbolea kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kusambaza kwenye mikoa mingine, kusambaza vitabu na vifaa vya maabara kwa Shule za Sekondari, kutoa ushauri majenzi kwa

Wizara na taasisi mbalimbali, kutoa huduma ya vipimo na tiba kwa wananchi kwa kushirikiana na Jeshi la Wanamaji la China na ujenzi wa ukuta kuzunguka machimbo ya madini ya Tanzanite-Mirerani Mkoani Manyara.

41. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama wa nchi yetu katika kupambana na matishio mbalimbali ya usalama yakiwemo ya ugaidi, biashara ya dawa za kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu, uvuvi na uwindaji haramu. Kwa kuwa, mashambulizi ya kigaidi yameendelea kuwa tishio la amani na usalama wa dunia, mafunzo ya kupambana na uhalifu huo na kubadilishana taarifa na uzoefu baina ya nchi na nchi yameendelea kufanyika. Hii ni pamoja na kujenga Kituo Maalum cha Mafunzo ya Kijeshi huko Mapinga, Bagamoyo.

Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana

42. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) limeendelea kutoa mafunzo kwa vijana wa kujitolea na wale wa Mujibu wa Sheria kwa lengo la kujenga uzalendo, ukakamavu na kutoa stadi za kazi. Katika mwaka 2017/18 JKT limeweza kuendesha mafunzo kwa vijana 11,388 kati yao wavulana 7,522 na wasichana 3,866. Aidha, JKT liliendesha mafunzo kwa vijana wa mujibu wa sheria 15,037 kati yao wavulana 10,348 na wasichana 4,689 waliohitimu kidato cha sita mwaka 2017. Lengo la JKT ni kuendelea kukarabati na kuanzisha makambi mapya ili kuwezesha kuchukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita.

43. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Jeshi la Kujenga Taifa pia liliendesha mafunzo kwa vijana 98 wa Wizara ya

Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuwajengea maadili mema, ukakamavu na moyo wa uzalendo kwa nchi yao. Aidha, Wizara na Taasisi zinakaribishwa kuleta maombi Makao Makuu ya JKT ili waweze kupangiwa muda wa kufanya mafunzo hayo. Taarifa tulizo nazo zinaonyesha kuwa vijana hawa wanafanya kazi vizuri zaidi baada ya mafunzo haya ikilinganishwa na hapo awali.

Mapambano dhidi ya UKIMWI

44. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza na kusimamia mikakati ya kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) kwa kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga ili kuzuia maambukizi mapya. Wizara imekuwa ikihimiza upimaji wa hiyari kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma na Vijana wa JKT kwa kutumia waelimishaji rika. Aidha, kwa wale ambao wamethibitika kuwa wameambukizwa Virusi vya Ukimwi wamekuwa wakipatiwa dawa za kupunguza makali ya Virusi (ARV's) bure katika vituo vya huduma na matibabu (Care and Treatment Centres) vilivyo katika Hospitali Kuu za Kanda na huduma ya lishe katika maeneo ya kambi. Pia, vituo hivyo hutoa huduma kwa wananchi wengine wanaoishi maeneo yaliyo karibu na kambi.

Utawala Bora

45. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza kwa vitendo dhana ya utawala bora kwa kuweka mifumo ya upimaji na matokeo ya utekelezaji wa mpango mkakati. Maafisa, askari na watumishi wa Umma wameendelea kuhimizwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya

utendaji kazi bila kusahau uzalendo, weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Katika utekelezaji wa dhana ya ushirikishaji katika mwaka 2017/18 mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi ilifanyika na masuala muhimu ya kiutendaji, utumishi na mengineyo yalijadiliwa na kukubalika ikiwemo ushiriki wa pamoja katika uandaaji na utekelezaji wa bajeti.

Utunzaji wa Mazingira

46. **Mheshimiwa Spika**, katika kushirika utunzaji wa mazingira, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kushirikiana na jamii katika kutunza mazingira katika maeneo yanayozunguka Vikosi vya Jeshi kwa kupanda miti. Kipekee JKT limeweza kupanda miti 26,000 katika maeneo ya chanzo cha maji Mzakwe na Chuo Kikuu cha Dodoma kuunga mkono kampeni ya kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kijani.

Matumizi katika Shughuli za Maendeleo

Ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi

47. **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2018 kati ya jumla ya **Shilingi 169,786,543,019.00** zilizopokelewa na Fungu 57 – Wizara zilitumika hasa kwa ajili ya ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi, na kiasi kingine kilitumika kununua malighafi kwa ajili ya kuongeza wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi katika Shirika la Mzinga na kuendeleza shughuli za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia pamoja na ukarabati wa baadhi ya miundombinu katika Shirika la TATC (Nyumbu).

Ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali

48. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fungu 38: NGOME **Shilingi 6,793,532,326.88** zilizopokelewa kwa ajili ya maendeleo zilitumika katika ujenzi wa ukumbi wa mihadhara (Auditorium) katika Chuo cha Ukamanda na Unadhimu-Duluti, Arusha, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya nyumba za makazi ya maafisa na askari pamoja na mahanga ya askari kapera katika Kamandi ya Wanamaji (Navy Command). Aidha, Jeshi limechangia ujenzi wa Kituo Maalum cha Mafunzo ya Kijeshi “Comprehensive Training Centre” (CTC) kilichopo Mapinga-Bagamoyo katika miundombinu ya umeme, maji, barabara za ndani na ujenzi wa uzio kuzunguka kituo hicho, pia kiasi kingine cha fedha kimetumika katika ujenzi wa ukuta wa Uwanja wa Ndege Vita Ngerengere.

49. **Mheshimiwa Spika**, Fungu 39: JKT lilipata **Shilingi 5,000,000,000.00** za maendeleo zilizotumika katika shughuli za ukarabati na ujenzi wa vikosi vipya, Makao Makuu ya JKT Chamwino-Dodoma, zahanati kwenye vikosi vipya, kuanzisha Kambi ya JKT Kibiti-Rufiji na ukarabati wa jengo la utawala katika Chuo cha Uongozi cha JKT kilichopo Kimbiji-Dar es Salaam.

Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT)

50. **Mheshimiwa Spika**, SUMAJKT limeendelea kutekeleza shughuli zake katika misingi ya kibiashara kupitia Kampuni Tanzu, Idara na miradi yake ifuatayo; Kampuni ya Ulinzi (SUMAJKT Guard Ltd), Kampuni ya Ujenzi (National Service Construction Department), Kampuni ya Ubia ya SUMAJKT - ANIT ASFALT CO.LTD, Idara ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo, Idara ya Viwanda na mradi wa matrekta.

51. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Ulinzi SUMAJKT Guard Ltd, inaendesha shughuli za ulinzi katika Ofisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Sekta binafsi zikiwemo Benki na Migodi. Kwa mwaka 2017/18 Kampuni imefanikiwa kuongeza huduma za ulinzi kwa taasisi za Serikali zipatazo 10 [Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Benki ya Posta Tanzania (TPB), Tanzania Global Learning Agency (TGLA) -Dar es Salaam, Wakala wa Misititu (TFS), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)- Bukoba, Mamlaka ya Elimu ya Vyuo vya Ufundi (VETA), Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, TEMESA Iringa, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)-Dar es Salaam, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)-Dodoma, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Wakala wa Barabara (TANROADS)].

52. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni imetoa mchango kwa Serikali kwa kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kuajiri vijana 5,063 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na vijana 4,150 mwaka 2016/17. Aidha, Kampuni imefanikiwa kununua magari matano ya doria na gari moja la kuzimia moto ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, Kampuni imekusudia kuimarisha shughuli zake kwa kuendelea kununua vitendea kazi vipya kama vile; vifaa vingine vya kupambana na moto na uokoaji, vifaa vya kudhibiti vurugu, vifaa vya kuhakikisha usalama katika usafirishaji fedha na magari ya kusafirishia wagonjwa ili kuongeza tija kwa shirika.

53. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa matreka mpaka sasa umesambaza matrekta 2,292 yenye thamani ya Shilingi 91,418,659,327.67 ambayo yaliuzwa kwa mkopo na fedha taslimu. Mpaka kufika Aprili, 2018 jumla ya Shilingi 53,181,022,212.51 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 51. SUMAJKT imekuwa

ikitumia vyombo vya habari kutoa matangazo kwa umma ya kuwataka wakopaji kulipa madeni yao ili mradi huu uwe endelevu. Aidha, mradi una mpango wa kununua matrekta 300 na majembe 500.

54. **Mheshimiwa Spika**, SUMAJKT, kupitia Kampuni ya Ujenzi (NSCD), limetekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa majengo na miundombinu ifuatayo; ujenzi wa Ukuta wa Machimbo ya Madini ya Tanzanite - Mirerani, ujenzi wa Bandari Kavu Kwala Vigwaza; ujenzi wa miundombinu ya Viwanda vya Sukari Morogoro; ujenzi na ukarabati wa majengo ya Halmashauri 23, Ujenzi na Ukarabati wa Shule za Serikali 16; ujenzi wa Kumbi mbili kwa ajili ya Sherehe na Mikutano za SUMAJKT na ujenzi wa Makao Makuu ya SUMAJKT Mkoani Dodoma.

55. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ya Shirika inashughulika na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, ufugaji na uvuvi. Mwaka 2016/17 Shirika lililima ekari 4,787 na kufanikiwa kupata tani 5,553. Katika mwaka 2017/18 Shirika limelima mazao ya chakula na biashara ekari 5,000 kati ya hizo, ekari 1,000 za mpunga, ekari 500 za maharage, ekari 300 za dengu, ekari 400 za alizeti na ekari 2,800 za mahindi. Shirika linatarajia kuvuna tani 6,450 kwa mazao hayo yote. Pia, Shirika lina jumla ya mifugo mbalimbali 9,794. Shirika limeendelea na ufugaji wa Samaki kwa njia ya Vizimba huko Rwamkoma, Mkoani Mara na kuanzisha mradi wa ufugaji wa Samaki kwa njia ya matenki (Re-circulating Aquaculture). Aidha, Shirika kupitia kampuni yake Tanzu ya SUMA JKT Seed Co. Ltd limeendelea na uzalishaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali.

56. **Mheshimiwa Spika**, katika masuala ya viwanda, SUMAJKT limeendelea kuimarisha viwanda vyake na kuanzisha viwanda vipya vifuatavyo; kiwanda cha maji ya kunywa na kiwanda cha ushonaji Mgulani, Mkoani Dar es salaam, Kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi Mlalakuwa, Mkoani Dar es Salaam, viwanda vya kuchakata nafaka Mafinga, Mkoani Iringa, Mlale, Mkoani Ruvuma na Kanembwa, Mkoani Kigoma. Aidha, Shirika lipo katika mchakato wa kuanzisha viwanda vifuatavyo; Kiwanda cha Maji ya Tiba (Intravenous fluid) na Kiwanda cha Dawa za Binadamu Kimbiji, Mkoani Dar es Salaam na Mradi wa Machinjio ya kisasa Ruvu Mkoani Pwani.

57. **Mheshimiwa Spika**, kupitia vyanzo vya mapato vya Shirika lake la Uzalishaji Mali la SUMAJKT, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kuchangia gharama za uendeshaji wa mafunzo ya vijana waliopo kwenye Kambi zake hivyo kuipunguzia Serikali mzigo.

Shirika la Mzinga

58. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Mzinga limeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya uzalishaji wa mazao ya msingi, ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa malighafi zinazopatikana hapa nchini ili ziweze kutumika katika uzalishaji na pia kufanya ukarabati wa zana na vifaa vya kijeshi. Aidha, kupitia Kampuni yake tanzu ya Mzinga Holding Co. Ltd, Shirika la Mzinga limefanikiwa kujenga hosteli ya chuo Kikuu cha Mzumbe, Mkoani Morogoro, kukamilisha ujenzi wa *Resource Centre*, Ifakara mkoani Morogoro, ujenzi wa Shule ya Msingi Camel, Uyole mkoani Mbeya na ujenzi wa wodi ya Wanaume katika hospitali ya Nyamagana, Mkoani Mwanza.

59. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Mzinga linaendelea kutekeleza jukumu la kusimamia zana na silaha zinazomilikiwa na makampuni ya ulinzi ambayo yanatoa huduma za ulinzi kwenye meli za kibiashara zinazoingia ndani ya mipaka ya nchi yetu. Aidha, meli ambazo hazitii nanga katika bandari yetu kutokana na muda mfupi wa meli hizo kukaa katika eneo letu hukaguliwa na kuhakikiwa zana na silaha walizonazo. Pia, kwa meli ambazo zinatia nanga katika bandari yetu kwa muda wa zaidi ya saa 24 hukaguliwa na zana huhifadhiwa na kurejeshwa kwenye meli masaa machache kabla ya kuondoka kwa meli hizo. Kazi hii inafanyika ili kudhibiti matumizi mabaya ya zana na silaha hizo.

60. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, Shirika limenunua malighafi za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya msingi. Aidha, Mpango Mkakati wa Shirika wa Miaka Mitano (2017/18 - 2021/22) unakusudia kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi. Pia, Shirika limepanga kuanzisha kiwanda cha kutengeneza baruti na kupanua mradi wa kutengeneza mashine ndogo ndogo kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali kuongezea thamani ya mazao ya kilimo na misitu.

Shirika la Nyumbu

61. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limetoa mchango mkubwa wa kupunguza matumizi ya Serikali kwa kushiriki katika maandalizi ya vifaa na zana za kijeshi kwa ajili ya ulinzi wa amani kwa kukarabati magari ya kivita, kutengeneza matela ya kubeba maji na mafuta, vitanda vya kulalia askari, mahema na majiko ya medani. Vilevile, Shirika limeshiriki kusimika na kukarabati miundombinu ya taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na

matengenezo ya mashine na mitambo kwa ajili ya matumizi ya JWTZ, vipuri vya viwandani pamoja na vitanda kwa ajili ya matumizi katika hospitali.

62. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Shirika limeendelea kutekeleza agizo la Serikali lililolitaka Jeshi letu kuongoza katika uanzishwaji wa viwanda nchini. Katika kuhakikisha kuwa Shirika linaendelea kutekeleza majukumu ya msingi ya kuanzishwa kwake, yameandaliwa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka kumi wa kuliimarisha Shirika ili liweze kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini. Mpango huu uko katika hatua za kuridhiwa na Serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 Shirika linatarajia kukarabati miundombinu ya majengo na mitambo iliyopo na kununua mitambo mingine ya kisasa, ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia, kwa lengo la kuongeza ufanisi na kukuza uwezo wa uzalishaji. Vilevile, Shirika limepanga kuanzisha kiwanda cha kutengeneza “air, oil na fuel filters” za magari, kiwanda cha kutengeneza betri za magari pamoja na kuanzisha karakana kuu ya matengenezo, upimaji na ukaguzi wa magari. Pia, Shirika limepanga kujenga kiwanda kikubwa cha kukalibu vyuma (foundry) kwa lengo la kuzalisha vipuri kwa ajili ya viwanda vyetu na sekta nyingine muhimu za uchumi, ulinzi na usalama, kilimo na usafirishaji. Hatua hii inatarajia kuliingizia Shirika mapato na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Mtandao wa Mawasiliano Salama Jeshini

64. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kupanua wigo wa mawasiliano Jeshini kupitia mradi wa Mtandao wa Mawasiliano Salama Jeshini. Katika mwaka 2017/18 Wizara imefanikiwa kuunganisha mawasiliano ya Mtandao huo kutoka Mkoa wa Morogoro hadi Dodoma. Hivi sasa, mawasiliano yanapatikana katika maeneo ya Dar es Salaam, Zanzibar, Pwani, Morogoro na Dodoma. Vilevile, Wizara inaendelea na mpango wa kupeleka mawasiliano haya katika mkoa wa Tanga. Aidha, jitihada za kuunganisha mawasiliano hayo katika vikosi vyote vya Jeshi vilivyosalia zinaendelea kufanyika.

Kudhibiti Uvamizi wa Maeneo ya Jeshi, Upimaji na Ulipaji Fidia

65. **Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uvamizi wa maeneo ya Jeshi, Wizara kupitia vikosi, vyo na shule za kijeshi, imeendelea kupanda miti, kuweka mabango kuzunguka maeneo hayo na kufanya doria za mara kwa mara kwenye mipaka ya vikosi. Aidha, Wizara imeweza kulipa fidia kwa ajili ya eneo la Shule ya Mafunzo ya Kijeshi Kihangaiko na juhudi za kulipa fidia katika maeneo mengine yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi zinaendelea kufanyika.

**CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI
KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

66. **Mheshimiwa Spika**, Wizara katika kutekeleza bajeti yake ya mwaka 2017/18 imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha ambapo kiwango kilichoidhinishwa cha **Shilingi 1,725,517,816,925.00** ni kidogo

ikilinganishwaa na mahitaji halisi ya **Shilingi 3,200,000,000,000.00**. Pia, kumekuwa na upungufu wa rasilimali watu katika baadhi ya Taasisi kama Mashirika ya Mzinga na TATC (NYUMBU). Aidha, bajeti iliyoidhinishwa kwa upande wa fedha za maendeleo zimekuwa zikitolewa kwa kiwango kidogo. Hali hii imesababisha kulegalega kwa utoaji wa huduma na Wizara kuendelea kuwa na madeni ambayo yana athiri utendaji wa Wizara na kupoteza uaminifu kwa wazabuni wanaotoa huduma na kuleta bidhaa mbalimbali.

67. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma ya uimarishaji na uanzishaji wa viwanda vipya Jeshini, zipo changamoto za uchakavu wa miundombinu (karakana, maabara, barabara, mitambo na majengo), teknolojia zilizopitwa na wakati, na upungufu wa watalaam wa kuendesha viwanda hivyo.

MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

68. **Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka 2018/19, unakusudia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa Jeshi katika kutekeleza majukumu yake kulingana na Dira na Dhima. Hivyo, Wizara imeazimia kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kulipatia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania vifaa na zana bora pamoja na kutoa mafunzo kwa wanajeshi ili kuliongezea uwezo wa kiutendaji kivita;
- ii. Kuboresha mazingira ya kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahili na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi raia,

- iii. Kuwapatia vijana wa kitanzania mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi;
- iv. Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa kuimarisha na kuanzisha viwanda kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia;
- v. Kuimarisha ushirikiano na Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na nchi moja moja katika nyanja za Kijeshi na kiulinzi;
- vi. Kutathmini na kulipa fidia ya ardhi katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi;
- vii. Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura pale inapohitajika;
- viii. Kuendelea kuendesha mafunzo na mazoezi kwa Jeshi la Akiba; na
- ix. Kuboresha mawasiliano salama Jeshini.

SHUKRANI

69. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watu mbalimbali kwa michango waliyotoa katika kutayarisha Makadirio haya. Nawashukuru Katibu Mkuu Dkt. Florens M. Turuka, Naibu Katibu Mkuu Bibi Immaculate P. Ngwalle, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Venance S. Mabeyo, Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali Yacoub H. Mohamed, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Martin S. Busungu, Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma.

70. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu

yangu. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

71. **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali napenda kuzishukuru Serikali za nchi mbalimbali, Mashirika na Wahisani kwa ushirikiano walioipatia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Wahisani hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Canada, India, Marekani, Ufaransa, Ujerumani na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za kiulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Bangladesh, Falme za Kiarabu, Ghana, Indonesia, Jamaica, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Morocco, Nigeria, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/19

Makadirio ya Mapato

72. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 75,420,100.00** kutoka katika mafungu yake matatu; ambapo Fungu 38-NGOME linakadiriwa kukusanya **Shilingi 17,317,100.00**, Fungu 39-JKT **Shilingi 56,903,000.00** na Fungu 57-Wizara **Shilingi 1,200,000.00**.

Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

73. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,910,722,891,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na

matumizi ya maendeleo ili iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2018/19. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,676,722,891,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 234,000,000,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo.

Mchanganuo kwa kila Fungu ni ufuatao:

Fungu 38 – NGOME

Matumizi ya Kawaida	Shilingi	1,364,232,770,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Shilingi	8,000,000,000.00
Jumla	Shilingi	1,372,232,770,000.00

Fungu 39 – JKT

Matumizi ya Kawaida	Shilingi	293,239,411,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Shilingi	6,000,000,000.00
Jumla	Shilingi	299,239,411,000.00

Fungu 57 – Wizara

Matumizi ya Kawaida	Shilingi	19,250,710,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Shilingi	220,000,000,000.00
Jumla	Shilingi	239,250,710,000.00

MWISHO

74. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa Hoja.

**UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA
MAPINDUZI 2015-2020**

Ibara 146 (i) Kuviwezesha vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha.

Maelezo:

1. Katika kufanikisha azma ya kuliongezea Jeshi rasilimali watu na rasilimali fedha, Serikali kupitia utaratibu wa Jeshi ilitoa **ajira mpya kwa vijana 3,000** waliopo katika kambi za JKT ili kujiunga na Jeshi. Utaratibu wa kuandikisha wanajeshi kutoka vijana waliopitia JKT ni endelevu kwani kwa kupitia utaratibu huu, Jeshi linapata askari vijana waliojengwa vyema kimaadili, uzalendo na ukakamavu kwa ajili ya kulitumikia Jeshi. Aidha, jumla ya Maafisa Wanafunzi **591** kati yao **534** wa kiume na **57** wa kike walitunukiwa **kamisheni** na Rais na Amiri Jeshi Mkuu Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli baada ya kuhitimu mafunzo na hivyo kuongeza wataalam katika Jeshi letu. Maafisa hao walipewa kamisheni tarehe 23 Septemba, 2017 na tarehe 3 Februari, 2018.

2. Katika kuwajengea uwezo Maafisa na Askari wake kiutendaji katika ngazi mbalimbali, Jeshi limetoa mafunzo kwa kozi mbalimbali kupitia Chuo cha Ulinzi wa Taifa (NDC), Ukamanda na Unadhimu (CSC- Duluti, Arusha), Chuo cha Kijeshi Monduli (TMA). Jeshi limetoa mafunzo kwa maafisa na askari kwa kozi mbalimbali za uongozi na taaluma za kijeshi, tiba, na utawala. Mafunzo haya yameliwezesha Jeshi kuongeza uwezo wake wa kiutendaji na utayari wa kivita (combat readiness). Aidha, mafunzo mengine yamefanyika nje ya nchi. Pia, programu mpya

ya “Bachelor of Military Science” imeanzishwa katika Chuo cha Kijeshi (TMA) Monduli mwaka 2017/18.

3. Ili kuimarisha uwezo wa kiutendaji kivita ikiwa ni pamoja na kushirikisha nchi rafiki, Jeshi limeshiriki mazoezi matatu ya Kimataifa yafuatayo: **Ex - Matumbawe** lililofanyika Mkoani Tanga kati ya tarehe 16 Julai na 30 Agosti, 2017 likihusisha nchi ya Tanzania, Zimbabwe, Afrika Kusini, Zambia, Malawi na Lesotho, **Ex - Blue Kunene** lililofanyika katika nchi ya Namibia kuanzia tarehe 24 Agosti hadi 2 Septemba, 2017 likishirikisha majeshi ya Anga kwa wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na **Ex - Ushirikiano Imara (CPX)** – 2017 lililofanyika kuanzia tarehe 4 - 20 Desemba, 2017 katika “Peace Keeping Training Centre” (PTC) – Kunduchi, Dar es Salaam likihusisha nchi za Afrika Mashariki.

4. Serikali imetoa fedha za ununuzi wa zana na vifaa kwa ajili ya Jeshi la Wanamaji na hivyo kuliongezea uwezo wa kufanya doria katika Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone-EEZ) na katika Operesheni za Kupambana na Uharamia na Uharibifu wa Mazingira.

Ibara 146 (ii) Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Maelezo:

Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya Wanajeshi wake kwa kuwapatia mishahara na posho mbalimbali kwa wakati kila mwezi, kuwapatia wanajeshi wote posho ya msahama wa kodi (Duty Free Allowance) ambayo inawezesha kila Mwanajeshi kunufaika badala ya wale waliopo katika maeneo ya mijini pekee kwenye maduka

hayo, kuandaa Mpango Bora wa Tiba kwa Wanajeshi wote na familia zao na kukamilisha miundombinu ya maji na umeme katika nyumba 6,064 kwa ajili ya makazi ya Wanajeshi katika vikosi vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Pemba, Kigoma na Kagera. Nyumba hizo zimeanza kutumika.

Ibara 146 (iii) Kuendelea kuweka mazingira mazuri yanayoliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha mafunzo kwa vijana wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa mujibu wa sheria.

Maelezo:

1. Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea vijana uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa pamoja na kutoa stadi za kazi kwa vijana wa kitanzania. Katika mwaka 2017/18 jumla ya vijana **26,393** walipatiwa mafunzo katika kambi mbalimbali hapa nchini. Kati yao vijana **15,037** ni wa mujibu wa sheria na vijana **9,848** ni wa kujitolea. Aidha, katika kipindi hicho, JKT lilitoa mafunzo kwa maafisa vijana **98** wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuwajenga katika maadili mema, ukakamavu na moyo wa uzalendo kwa nchi yao.

2. Jeshi la Kujenga Taifa limefanikiwa kufanya ukarabati na ujenzi katika vikosi vipya, Makao Makuu ya JKT Chamwino-Dodoma, zahanati kwenye vikosi vipya, kuanza maandalizi ya kuanzisha kambi mpya ya JKT Kibiti-Rufiji na ukarabati wa jengo la utawala katika Chuo cha Uongozi cha JKT kilichopo Kimbiji-Dar es Salaam. Aidha, katika kuongeza motisha ya utendaji kazi JKT, mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 umehusisha pia ujenzi wa

nyumba katika kambi za JKT ambapo maafisa na askari wa Jeshi hilo wamegawiwa. Kwa upande wake Wizara inaendelea kuliwezesha JKT kufikia malengo ya kuchukua vijana wengi zaidi kulingana na upatikanaji wa fedha.

3. Katika kutekeleza azma ya kupunguza gharama za uendeshaji, JKT limetenganisha shughuli za uzalishaji mali zinazosimamiwa na SUMAJKT na shughuli za mafunzo kwa vijana wanaojiunga na JKT kwa mujibu wa sheria na wa kujitolea. JKT limeendelea kutumia rasilimali zake katika kuhudumia na kutoa mafunzo kwa vijana wanaojiunga na mafunzo hayo, ikiwa ni pamoja na kuchangia gharama za chakula kwa kuzalisha chakula hicho katika kambi zake. Kwa upande wake SUMAJKT limeendelea kujiendesha kibiashara ili kupata faida na kuchangia gharama za kuliendesha Jeshi la Kujenga Taifa.

Ibara 146 (iv) Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika shughuli za Ulinzi wa Amani kwenye nchi mbalimbali duniani ili majeshi yetu yaendeleo kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani.

Maelezo:

1. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushiriki katika Operesheni za kimataifa na kikanda chini ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na chini ya Jumuiya za Kikanda. Jeshi limeshiriki shughuli za ulinzi wa amani katika Jimbo la Darfur nchini Sudani, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ambako Jeshi limepeleka kikosi kikiwa ni sehemu ya Jeshi la kulinda amani nchini DRC- MONUSCO (Force Intervention Brigade - FIB). FIB inashirikisha nchi tatu wanachama wa SADC ambazo ni Tanzania, Malawi na Afrika Kusini. Aidha, Jeshi limetuma kikosi

kwa ajili ya kulinda amani katika Jamhuri ya Afrika ya Kati na Polisi Jeshi nchini Lebanon. Jeshi linategemea kupeleka Kombania ya wahandisi wa medani (Combat Engineers) nchini Sudani Kusini baada ya kukamilika kwa makubaliano ya kimkataba (Memorandum of Understanding) baina ya Serikali ya Tanzania na Umoja wa Mataifa.

2. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jeshi limeshirikiana na nchi wanachama kwa kufanya mazoezi mbalimbali ya ushirikiano ikiwemo Zoezi Ushirikiano Imara lililofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 20 Desemba, 2017 Kunduchi, Dar es Salaam. Aidha, katika kuendeleza ushirikiano, Jeshi lilishiriki michezo ya Majeshi iliyofanyikia nchini Burundi. Kuhusu Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Jeshi limeendelea kushirikiana na nchi wanachama kwa kufanya mazoezi ya pamoja. Katika mwaka 2017/2018, JWTZ lilikuwa mwenyeji wa **Zoezi Matumbawe 2017** (SADC Special Forces) lililofanyikia mkoani Tanga. Zoezi hilo liliongeza uwezo wa Jeshi katika kupambana na wahalifu ndani na nje ya nchi.

3. Katika kuendeleza mahusiano ya kijeshi na nchi mbalimbali na kuzuia matishio ya utekaji meli katika Bahari ya Hindi, Jeshi limekuwa likishirikiana na nchi za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Australia, Bangladesh, China, Hispania, India, Iran, Italia, Pakistan, Sierra Leone, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza na Urusi, kuzuia uharamia katika Bahari ya Hindi.

Ibara 146 (vi) Kuendelea kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka (Cross Border Crimes) hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji wa fedha haramu (money laundering), biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji wa binadamu.

Maelezo:

Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Wananchi, vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama na mataifa mengine katika kupambana na matishio ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uvuvi haramu, uharamia, biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji wa binadamu. Ushirikiano huu umeliwezesha JWTZ kupata uzoefu na kujifunza mbinu mpya za kupambana na wahalifu wa makosa hayo.

KIAMBATISHO NA. 2

MCHANGANUO WA BAJETI NA KIASI KILICHOPOKELEWA HADI MWEZI APRILI, 2018

Fungu	Matumizi Yaliyoidhinishwa	Bajeti ya Mwaka 2017/18	Kiasi Kilichopokelewa	Asilimia
38	Mishahara	925,168,039,000.00	771,643,973,582.10	83.41
	Chakula	198,000,000,000.00	155,525,800,000.00	78.55
	Matumizi Mengineyo	24,611,250,563.00	62,511,287,697.00	254.00
	Maendeleo	8,000,000,000.00	6,793,532,326.88	84.92
	Misamaha ya Kodi	57,465,000,000.00	43,366,500,000.00	75.47
	Jumla ya Fungu	1,213,244,289,563.00	1,039,841,093,605.98	85.71
39	Mishahara	167,218,788,380.00	144,422,936,226.50	86.37
	Chakula	65,231,688,000.00	48,666,493,000.00	74.61
	Matumizi Mengineyo	26,919,054,403.00	23,525,864,206.90	87.39
	Mafunzo ya vijana wa Mujibu wa Sheria	12,500,000,000.00	7,217,797,384.00	57.74
	Posho ya Msamaha wa kodi	11,493,000,000.00	8,619,750,000.00	75.00
	Maendeleo	6,000,000,000.00	5,000,000,000.00	83.33
	Jumla ya Fungu	289,362,530,783.00	237,452,840,817.40	82.06
57	Mishahara (Wizara na Mashirika)	11,734,491,000.00	8,331,481,300.00	71.00
	Ruzuku (Mashirika na Majenerali)	4,730,141,000.00	3,058,819,400.00	64.67
	Matumizi Mengineyo	1,446,365,000.00	1,712,452,000.00	118.40
	Madeni mbalimbali	0.00	114,620,000.00	
	Maendeleo	205,000,000,000.00	169,786,543,019.00	82.82
Jumla ya Fungu	222,910,997,000.00	183,003,915,719.00	82.10	
	JUMLA KUU	1,725,517,817,346.00	1,460,297,850,142.38	84.63